Jarida la

# MADINI & UCHUMI

Online Bulletin

WWW.MADINI.GO.TZ | TOLEO LA 05 | JUNI, 2022

JARIDA MTANDAONI



# TUMEJIPANGA KUTEKELEZA VIPAUMBELE VYA WIZARA



Dkt. Doto .M. Biteko
**Waziri wa Madini**

Napenda kutumia ukurasa huu kuwafahamisha na kuwahakikishia wadau wa madini na watanzania wote kuwa, katika Mwaka 2022/23 wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele vyake ambavyo vinalenga kuhakikisha rasilimali madini zinazidi kulinufaisha taifa letu kiuchumi na kimaendeleo kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26, Sera ya Madini ya Taifa 2009, mpango mkakati wa wizara wa mwaka 2019/20-2023/24 na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025.

Vipaumbele ambavyo wizara imepanga kutekeleza Mwaka wa Fedha 2022/23 ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki uchumi wa madini; kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini. Vipaumbele vingine ni pamoja na kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya wizara na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi

Nikitaja tu kwa uchache, utekelezaji wa vipaumbele hivyo utahusisha utekelezaji wa mikakati mbalimbali ikiwemo kufungua na kusimamia migodi mikubwa na ya kawaida ya uchimbaji madini ya kinywe (graphite) pamoja na kuhakikisha migodi yote mikubwa inaajiri watanzania na kununua bidhaa huduma na bidhaa kutoka hapa nchini kwa kiwango cha kuridhisha kwa kadri ya upatikanaji wake na kutoa huduma za kijamii katika maeneo husika.

Pia, ili kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa Madini, wizara imepanga kuendelea kuwatengea maeneo au kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo yana taarifa za msingi za kijiolojia, kutoa huduma za utafiti kwa gharama nafuu; kuwaendeleza wachimbaji wadogo kuwa wa kati na hatimaye kuwa wakubwa ikiwemo kuwapa mafunzo yanayohitajika kuhusu uchimbaji, uchenjuji na biashara ya madini.

Aidha, kama mtakumbuka, serikali imekuwa ikisisitiza na kuweka jitihada za kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani madini zinafanyika nchini, katika mwaka wa fedha ujao, wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; na kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini

Aidha, wizara katika mwaka ujao itaendelea kuhamasisha biashara na uwekezaji katika sekta ya Madini kwa kuweka mazingira yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini bila kuathiri ustawi na matarajio ya nchi kutokana na uwekezaji huo. Pia, wizara itabuni na kutekeleza mikakati ya kuthaminisha uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kufanya tafiti za madini ya kimkakati, madini ya viwandani ya metali; kujenga Imani kwa biashara ya madini nchini kwenye uwanja wa kimataifa kwa kutekeleza wajibu wa nchi kama wanachana wa Extractive Industries Transparency Initative (EITI). Wizara pia itashighulikia changamoto zote zilizojitokeza mwaka 2021/22 ili kuhakikisha inaondoa aina zote zinazoweza kukwaza utendaji wa wadau wote wa Sekta ya Madini.

Rai yangu kwenu wadau wa madini tuendelee kushirikiana kwa kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kikamilifu kwa kufuata Sheria, Taratibu na kanuni zilizopo wakati tunapotekeleza majukumu yetu ili kuiwezesha sekta yetu iendelee kukua na kuchangia ipasavyo kwenye Pato la Taifa na hatimaye tuweze kufikia lengo letu la kufikia asilimia 25 ya mchango wa sekta yetu kwenye Pato la Taifa.

Pia, naendelea kuwakumbusha wadau wote wa Sekta ya Madini kushiriki kikamilifu katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika mwezi tarehe 23 Agosti, 2022. Kama mtakumbuka, katika Sensa itakayofanyika mwaka huu, itahusisha kipengele maalum kitachohusu masuala yanayohusu wachimbaji wadogo. Hivyo, ushiriki wetu, utaiwezesha Serikali kupanga mipango ya maendeleo kikamilifu katika sekta yetu ya Madini.

**SHIRIKI NA JIANDAE KUHESABIWA KATIKA SENSA YA WATU NA MAKAZI KWA MAENDELEO YA SEKTA YA MADINI**

# UJUMBE WA KATIBU MKUU

## TUMEMALIZA MWAKA WA FEDHA 2021/22 KWA MAFANIKIO



Adolf Ndunguru

**Katibu Mkuu - Wizara ya Madini**

Tumemaliza Mwaka wa Fedha 2021/2022 huku mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa ukiendelea kuimarika na nchi yetu ikiendelea na inayotarajiwa kufunguka kiuchumi kupitia uwekezaji mkubwa kufanyika nchini.

Mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa umeendelea kuimarika ambapo katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2021, uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.3 kutoka wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, katika robo ya mwaka ya Julai hadi Septemba 2021 mchango wa sekta uliongezeka hadi kufikia asilimia 7.9 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 7.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2020.

Aidha, katika Mwaka huo wa Fedha tulishuhudia taifa letu likiandika historia mpya za kiuwekezaji baada ya kutolewa kwa Leseni kubwa ya uchimbaji mkubwa wa Madini ya Nikeli kwa Kampuni ya Tembo Nickel Corporation Limited na kusainiwa kwa mikataba mbalimbali ya kuchimba madini kupitia Leseni kubwa na za kati.

Uwekezaji kupitia Leseni ya Tembo Nickel iliyotolewa Oktoba 27, 2021, inatarajia kulipatia taifa letu mapato ya Dola za Marekani Bilioni 7.54 sawa na shilingi Trilioni 17.35 yatakayopatikana katika kipindi chote cha utekelezaji miradi kupitia kampuni hiyo ambayo ni ya ubia kati yake na Serikali. Serikali ikiwa na hisa asilimia 16 na mbia asilimia 84.

Desemba 13, 2021, Serikali ilisaini mikataba minne (4) kwa wakati mmoja kati yake na kampuni za madini za Sotta Mining Limited, Jacana Resources Limited (Strandline Resources) Black Rock Resources (Mahenge Resources) na kampuni ya Williamson Diamond Limited ambayo serikali imeongeza umiliki wa hisa zake kutoka asilimia 25 hadi 37. Thamani ya uwekezaji kwa kampuni hizo zitakazochimba madini ya dhahabu, kinywe, madini mazito ya machanga wa baharini na madini ya almasi ni dola za Marekani milioni 735.79.

Utekelezaji wa shughuli hizo utaendelea kulipatia taifa letu mapato yatokanayo na kodi, ajira, kurithisha teknolojia za kisasa, utaalamu, kuendelea kuvutia mitaji mingine na kuendelea kuongeza mchango wa sekta ya madini.

Kwa upande wa masoko ya madini, yamezidi kuongezeka tangu kuanzishwa kwake kufikia masoko 42 na vituo vya ununuzi wa madini 75. Kuongezeka kwa idadi ya masoko hayo na uwepo wake umeimarisha kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na Sekta hii ambapo katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 shilingi bilioni 416.6 zimekusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wa wachimbaji wadogo, wizara imewawezesha wachimbaji wadogo kushiriki uchumi wa madini kwa kuzihamasisha taasisi za fedha na mabenki nchini kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo, lengo ni kuwawezesha wakue na wachimbe kwa tija. Hadi sasa baadhi ya benki zikiwemo za NMB, NBC, CRDB na KCB zimeridhia na kuanza kutoa mikopo ambapo jumla ya shilingi bilioni 36 zimekopeshwa kwa wachimbaji wadogo. Hizi ni juhudi ambazo serikali ilizitaka za kuhakikisha wachimbaji wanakua, wanashiriki uchumi wa madini na kuchangia katika Pato la Taifa.

Haya ni baadhi tu ya mafaniko machache ambayo wizara imeyatekeleza katika kipindi cha mwaka huu wa fedha yakilenga kuhakikisha rasilimali madini inatumika kuleta maendeleo na wananchi wanakuwa sehemu ya washiriki wa uchumi huu.

Ni adhima yetu na tumejipanga kutekeleza mipango iliyo mbele yetu kwa kipindi cha mwaka wa fedha ujao kwa kutatua changamoto zilizojitokeza huko nyuma ili kuhakikisha wadau wote wa Sekta ya Madini wanapata manufaa tarajiwa.

**SHIRIKI NA JIANDAE KUHESABIWA KATIKA SENSA YA WATU NA MAKAZI KWA MAENDELEO YA SEKTA YA MADINI**



# MWAKA 2021/22 ULIVYOONGEZA TIJA SEKTA YA MADINI

**Na Asteria Muhozya**

Wizara ya Madini imekamilisha utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kukiwa na matokeo makubwa kwenye sekta ya Madini na kuwa mfano kutokana na maendeleo yaliyopigwa na hivyo kupelekea baadhi ya mataifa kuja nchini kujifunza kupitia ziara, mikutano na kupata nafasi ya kushiriki katika majukwaa ya kimataifa.

Mfano dhahiri ni idadi ya nchi zilizoshiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini uliofanyika mwezi Februari, 2022, ambapo wizara ilipokea mawaziri na wawakilishi kutoka nchi tisa (9) walioshiriki katika mkutano huo ukiachia mbali wale walioshiriki kwa njia ya mtandao. Nchi zilizoshiriki moja kwa moja ni Sudan ya Kusini, Sudan, Uganda, Visiwa vya Comoro Burundi, Zambia, Zimbabwe, Libya na Kenya. Wageni hao walivutiwa na mkutano na walikiri kujifunza mengi kupitia mkutano huo kuanzia kwenye Sheria inayosimamia Sekta, mnyororo mzima wa biashara ya madini, namna sekta inavyoshirikisha wadau, inavyowaendeleza wachimbaji wadogo na kadhalika.

Aidha, mara baada ya mkutano huo, Mawaziri kutoka nchi za Burundi na Zimbabwe walitembelea Tanzania kwa lengo la kujifunza masuala yanayohusu usimamizi wa sekta ya Madini ikiwemo uwekezaji mkubwa unaotarajiwa kufanyika mathalan kwenye uchimbaji wa madini ya nikeli, uwekezaji katika kiwanda cha kusafisha dhahabu, biashara ya madini kupitia Masoko ya Madini na namna Tanzania ilivyosaidia kukuza sekta ndogo ya uchimbaji mdogo wa madini.

Akizungumza katika ziara yake nchini hivi karibuni, Naibu Waziri wa Madini na Uendelezaji Migodi wa Zimbabwe Dkt. Polite Kambamura anakiri kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika eneo la usimamizi wa shughuli za uchimbaji mdogo wa madini suala ambalo linafanya nchi hiyo kuja kujifunza. Anasema kuwa, mfumo uliojengeka kwenye sekta ya Madini ni wa uwazi kuanzia kwenye uchimbaji, usafishaji, usafirishaji na namna inavyothibiti utoroshaji wa madini.

Uchimbaji mdogo ni moja ya maeneo ambayo serikali imeweka jitihada ya kuhakikisha wachimbaji wadogo wanakua na kuchimba kwa tija. Kufuatia hali hiyo, katika mwaka 2021/22, wizara iliendelea kuzihamasisha taasisi za fedha na benki nchini zikiwemo NMB, NBC, CRDB na KCB kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo. Hadi sasa baadhi ya benki hizo zimeridhia kutoa mikopo ambapo jumla ya shilingi bilioni 36 zimekopeshwa kwa wachimbaji wadogo. Kadhalika, baadhi ya benki zimeahidi kutoa mikopo ya vifaa kwa wachimbaji wadogo.

Mbali na hatua hizo, pia, wizara kupitia taasisi zake za Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) katika mwaka 2021/22 ziliendelea

kutoa elimu ya uchimbaji bora, utafiti, uchejuaji bora, biashara ya madini kuhakikisha wachimbaji wadogo wanakua kutoka katika uchimbaji mdogo.

Pia, mbali na wizara kutembelewa na wageni kwa lengo la kujifunza, pia, wizara ilipata mialiko ya kuhudhuria majukwaa ya kimataifa na maonyesho makubwa ambapo ilitoa uzoefu wake wa usimamizi wa sekta na kunadi fursa zake za kiuwekezaji zilizopo kwenye sekta. Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko aliongoza timu ya wataalam wa wizara na taasisi kushiriki katika Kongamano la uwekezaji na Biashara ya Madini lililokwenda sambamba na maonesho makubwa ya madini yanayohusisha wazalishaji na watumiaji wa bidhaa za madini duniani (PDAC) nchini Canada. Katika kongamano hilo, waziri Biteko alitoa mada kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo kwenye sekta ya Madini katika eneo la utafutaji, madini, uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini na shughuli za kutoa huduma migodini. Pia, Tanzania ilishiriki katika jukwaa la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Italia nchini Italia na kongamano la madini na teklonojia nchini Saudi Arabia. Vilevile Wizara ilishiriki kwenye Kongamano la Uwekezaji kwenye Sekta ya Madini kwa nchi za Afrika (Investing in African Mining INDABA).

Naye, Naibu Waziri wa Madini Dkt. Steven Kiruswa alishiriki katika mkutano wa Uwekezaji katika Rasilimali za Madini na Mafuta nchini Nigeria ambapo wizara ilitoa wasilisho katika mkutano huo kuhusu maendeleo ya sekta, fursa zilizopo na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali za kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi ambapo Dkt. Kiruswa alieleza kuwa tayari Tanzania imeanza kuchukua hatua hizo kwa kuanzisha migodi ya madini ya nikeli na kinywe (graphite) ambayo hutumika hutengeneza magari yasiyotumia mafuta.

Vilevile, sekta ya Madini ilishiriki katika maonesho makubwa ya Expo 2020 Dubai na kupewa kipaumbele katika banda la Tanzania kutokana na utajiri wa maliasili za madini zilizopo nchini. Katika maonesho hayo, sekta ya Madini ilikuwa kivutio katika banda la Tanzania kutokana na fursa za kiuwekezaji zilizopo ambazo zilichochewa na taarifa za kijiolojia za GST. Aidha, katika maonesho hayo, STAMICO ilisaini mkataba wa ushirikiano katika utafiti na uendelezaji leseni kati ya STAMICO na kampuni ya ACME Consultancy Engineers Pte Ltd wenye thamani ya takriban dola za Marekani milioni 300.

Aidha, wizara ilikuwa mwenyeji katika kikao cha Kamati ya Ukaguzi wa Umoja wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) kilichofanyika mkoani Kagera. Kamati hiyo ilichagua kufanyia kikao nchini ikilenga pia kujifunza namna biashara ya Madini ya bati (TIN) inavyofanyika kupitia soko lake lilipo wilayani Kyerwa. Nchini Tanzania, madini ya Bati yanachimbwa kwa wingi mkoani Kagera. Aidha, tayari Tanzania ina kibali cha kufanya biashara ya madini hayo mahali popote ulimwenguni baada ya kupata cheti cha ithibati kilichotolewa mwaka 2020 kinachoonesha kwamba imekidhi vigezo vya kuuza madini hayo.

Kuhusu mchango wa sekta ya Madini kwa mwaka 2021/22 kwenye Pato la Taifa uliendelea kuongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2020 hadi kufika asilimia 7.2 mwaka 2021 na kuifanya Sekta ya Madini kushika nafasi 5 miongoni mwa sekta nyingine za kiuchumi. Mathalan, mwaka 2021 sekta ya Madini imechangia asilimia 45.9 ya thamani ya bidhaa zote zilizouzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa dola za Marekani milioni 3,103.20. Aidha, kasi ya ukuaji mwaka 2021 ilikua kufikia asilimia 9.6 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2020 na kuwa ya tatu miongoni mwa sekta nyingine kutokana na ongezeko la uwekezaji.

Pamoja na mapato yaliyotokana na maduhuli na fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini nje ya nchi, pia, sekta ya Madini iliiwezesha Serikali kukusanya shilingi trilioni 1.58 kutoka vyanzo mbalimbali vya kodi mwaka 2021 ikilinganiswa na shilingi trilioni 1.34 mwaka 2020 ongezeko hilo likiwa ni sawa na asilimia 17.9.

Pamoja na hayo yaliyoanishwa, yapo mengi yaliyotekelezwa katika kipindi cha Mwak wa Fedh 2021/22 ambayo yameongeza tija katika ukuaji na maendeleo ya sekta ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Ni matumaini ya safu hii






# TEMBO NICKEL GATHERS MOMENTUM FOR DEVELOPMENT OF TANZANIA'S CLASS 1 NICKEL MINE

**By Sauda Simba- Tembo Nickel**

As the Ministry of Minerals closes its Financial Year 2021/22, it can look back on its stakeholder's projects and reflect on the milestones achieved on the path to achieving its goal of 10% GDP contribution to the national economy by 2025.

Tembo Nickel's Kabanga Nickel Project is a major one on the radar, being the largest development-ready nickel sulphide project in the world. This is the next big project out of Tanzania, projected to start production of Class 1 nickel in early 2026.

Alongside the mine will be a refinery at Kahama which will use a new technology, namely hydrometallurgy. This method is more cost efficient than traditional smelting and has significantly lower environmental impact. Kahama is an ideal location for the refinery given the proximity to power and logistics.

Since the signing of the Framework Agreement between Kabanga Nickel Limited and the Government in January 2021, to form the partnership operating company Tembo Nickel, and the issue of the Special Mining License for the Kabanga Nickel Project in October 2021, Tembo Nickel has hit the ground running.

The strategic project was able to attract the mining giant BHP committing to an investment of 100 million dollars, starting with disbursement of the first 50 million dollars of which 40 million dollars is going to accelerate the project development and 10 million dollars to progress the low carbon hydrometallurgical processing technology for the refinery.

Tembo Nickel's metallurgical drill program has now been completed and further infill exploration is in plan to increase the ore body resource and better define the ore classification for mine planning purposes.

The high grade of the nickel in the Kabanga project is "the sweet stuff" for auto manufactures as described by Kabanga Nickel Chief Executive Officer Chris Showalter its configuration is the exact material that the electric vehicle manufactures are looking for. This premium nickel will be highly sought after for lithium-ion batteries needed in electric cars, meaning that the product coming out of Tanzania once production begins, puts Kabanga Nickel in an enviable position to negotiate for the best




Bugarama Primary School, World Environment Day parade.

off-take agreements. It also means that Tanzania has a huge part to play in the global energy transition and decarbonization goals," describes Showalter.

Showalter's statement is supported by Minister for Minerals Dr. Doto Biteko Minister Biteko saying Tanzania has the potential to develop a modern green economy producing finished metals that are critical for the world to transition to net zero. "At the center of this vision proudly sits Tembo Nickel" he said.

The Kabanga refinery will be a game changer and Kabanga Nickel CEO Chris Showalter says the company intends to be able to provide for multiple other mining operations in Tanzania and also as part of the government's vision to make the country the value addition center in the East Africa Region." Full beneficiation of nickel will be carried out in country and will maximize the country's value addition capability.

Tembo Nickel has also begun the ESIA update program that includes the environmental management plan and engaging all the relevant stakeholders in the process. It is expected that this will be completed over the next seven to eight months.

Due to its potentiality, in May 2021, the Kabanga project was visited by Burundi Minster for Energy Eng. Ibrahim Uwizeye to learn more about the project. identify opportunities as well as synergies for his country's potential nickel projects.

"Burundi has large deposits of nickel at Muremela and Msongati, there is a need to borrow a leaf from Tanzania's mining experience" He expressed.

Tembo Nickel also attended the Mining Indaba Conference in Cape Town in May with the theme – The evolution of African Mining: Investing in the Energy Transition, ESG, and the economies. ESG and sustainably are core to the Kabanga Nickel Project

In the meantime, Tembo Nickel has supported the District Commision Office which engaged Atansio Andrew the district environmental officer to sensitize all village leadership and members of the communities in all 6 communities surrounding of mine area on village environmental law. These villages are Bugarama, Nyabihanga, Mukubu, Muganza and Rwinyana. The leaders and the community surrounding the mine site area were made aware of their responsibility to the environment, as leaders and community in the area, they gained important knowledge on the governing environmental laws.

Leading up to June 5th, World Environment Day, Tembo Nickel sponsored a clean up and the supply of over 400 avocado seedlings to Rwinyana and Bugarama primary schools and the dispensary.

A social license to operate is central to ensuring smooth operations and Tembo Nickel continues to build strong relations with the communities surrounding the mining area, as well as at district, regional and national levels. In preparation for the land acquisition and resettlement program, Tembo Nickel supported the District Commisioner's office on two major sensitization programs, namely operation "Ondoa Tegesha Ngara" which focused on addressing speculators

infiltrating the project area. Secondly Tembo Nickel supported the engagement of a district land officer, Cosmas Rubambura to sensitize village leadership and the surrounding six villages in the licensed area about their rights and responsibilities around land issues.

Tembo Nickel is also working closely with resettlement consultants to oversee the land and asset survey and to ensure that site is fairness and in compliance with the requirements of the law.

The community development support is a legal requirement stipulated in the Mining Act 2018 Section 105 referred to as Corporate Social Responsibility ("CSR"). Tembo Nickel's approach to CSR and community development is woven into its strategic objectives and recognizes that sustainability of the environment and communities starts today. Investing today and into the future needs to have a local, regional and national impact. This reaches across development programs, training, job creation, support and stimulation of business. Overall having a significant contribution to the national GDP.

In the past financial year close to 40 million shillings was provided as an extension of the previous operator Kabanga Nickel Corporation Limited's support. It covered 11 projects, 7 infrastructure construction projects of 6 primary schools and 1 secondary school. In addition, 3 equipment supply projects to 1 primary school and 2 dispensaries as well as a capacity building project. The capacity-based program is a community health worker refresher training program to 18 community health workers, 2 from each project affected village. There was also support for popular national and international events. This year's budget is close to 208,000,000 shillings, focusing mainly on schools and dispensaries. All these programs are selected in a totally transparent and participatory manner and prioritized by the community.

Tembo Nickel has committed to creating jobs to qualified Tanzanians and is beginning to fulfill this promise. This year 16 new staff were recruited for the Relocation Action Program and Camp management. 90% recruits are from the Ngara area. After the mine and refinery build, it is projected that there will be around 900 employed at the mine site and 300 at the refinery. Tembo Country Manager Benedict Busunzu has pointed out that "beyond the money, having a mining giant like BHP partnering with us brings both transfer of skills and experience".

In keeping with the requirements of the mining law Tembo Nickel has ensured that is sources its products and services locally as much as possible. 98% of total supplies have been sourced locally with only 2% internationally, whereas 79% of services have been sourced locally and the remainder 21% internationally. 92% of good are sourced in country but outside of Ngara and 8% in Ngara.





# MADINI YA TANZANIA KUILISHA DUNIA

**Na Asteria Muhozya**

Tanzania ni miongoni mwa nchi 191 zilizoshiriki Maonesho ya Dunia ya Expo 2020 Dubai ambayo hufanyika kila baada ya miaka mitano. EXPO ni Maonesho Makubwa ya Dunia ambayo huchukua takribani miezi mitatu (03) hadi sita (06) na huratibiwa na Shirikisho la Maonesho Duniani (Bureau of International Expositions – BIE). Katika Maonesho haya nchi Wanachama wa BIE hupiga kura ili kuchagua nchi itakayokuwa mwenyeji wa EXPO, ambapo wapiga kura huwa ni nchi zilizo wanachama wa Shirikisho. Makao Makuu ya BIE yapo katika mji wa Paris nchini Ufaransa.

Katika maonesho ya mwaka 2020 yaliyofanyika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu, Dubai ilikuwa mwenyeji na ilitenga eneo maalum kwa ajili ya maonesho lililojulikana kama Expo 2020. Mitaa ndani ya eneo tengefu ilipangwa kulingana na kaulimbiu ndogo ndogo zinazohamasisha Kusongambele, Fursa na Uendelevu (Mobility, Opportunity and Sustainability), hii iliwapa nchi washiriki fursa ya kujitangaza kulingana na kaulimbiu hizo. Maonesho hayo hulenga kuzipatia nchi washiriki fursa ya kujifunza kutoka nchi nyingine ikiwemo kutangaza fursa za teknolojia na uwekezaji.

Kaulimbiu kuu katika maonesho hayo ilisema Fikra za Pamoja, Hujenga hatma ya baadaye. "Connecting Minds, Creating the Future", ililenga kuleta fikira za pamoja kwa lengo la kupata ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikabili dunia. Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi zilizoshiriki maonesho hayo, katika eneo la mobility ilikuwa na kaulimbiu ndogo ya "Connectivity, Tanzania Ready for Take Off". Kaulimbiu hiyo inaonesha utayari wa Tanzania kuwa Kitovu cha Biashara Barani Afrika ili kuiunganisha Afrika na Dunia.

Kwa upande wa Tanzania, mbali na Sekta ya Madini, Nishati, Utalii, Kilimo, Miundombinu, taasisi za umma na binafsi ni miongoni mwa sekta zilizoshiriki katika maonesho hayo. Sekta ya Madini ilipewa kipaumbele katika banda la Tanzania kutokana na utajiri wa rasilimali za madini ambayo nchi imebarikiwa kuwa nayo. Miongoni mwa madini hayo ni metali, nishati, viwandani na vito. Aidha, kuna fursa mbalimbali za kibiashara na kiuwekezaji zilizopo nchini kupitia sekta hiyo. Kulionekana kuwa na uhitaji wa madini ya Tanzania ambapo kampuni mbalimbali zilizoshiriki na kutembelea banda la Tanzania ziliomba kukutana na wataalam wa Sekta ya Madini, ili kupatiwa taarifa za kina za kijiolojia, taratibu za uwekezaji na biashara ya madini ambapo kampuni hizo zilivutiwa na mazingira ya uwekezaji kwenye sekta ya madini.

Madini ya kimkakati yanayopatikana Tanzania yakiwemo ya colbat, nikeli, kinywe (Graphite), Rare Earth Elements (REE), urani, madini ya helium, madini ya mchanga mzito wa baharini (heavy mineral sands) na mengineyo yalionekana kukuhitajika sana duniani, kwa ajili ya matumizi ya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali hususan matumizi ya kielektroniki na teknolojia. Kamishna Jenerali wa Banda la nchi ya Marekani Bw. Robert Clark anathibitsha hilo baada ya kufurahishwa na ushiriki wa Sekta ya Madini, alipotembelea banda la Tanzania. Kamishna huyu aliahidi kuiunganisha Tanzania na wawekezaji wa madini ya cobalt pamoja na wawekezaji wengine na kueleza kuwa, madini ya kimkakati ya Tanzania ni suluhisho kwa nchi yake na dunia.

Pia, zipo kampuni zilizoonesha nia ya kushirikiana na Tanzania katika biashara ya madini ya kimkakati. Miongoni mwa kampuni hizo ni Kampuni ya Elves Graphite ya Korea Kusini iliyoonesha nia ya moja kwa moja huku ikiomba

kupata usaidizi wa haraka wa taratibu zinazohusu shughuli za uchimbaji au ununuzi wa madini ya kinywe ambayo utumika kwa wingi katika kampuni nchini humo. Kampuni hii iliitaja kampuni ya SAMSUNG kuwa miongoni mwa watumiaji wakubwa wa madini hayo. Aidha, mwakilishi wa banda la Slovakia alionesha kuuona upekee wa Tanzania baada ya kupatiwa taarifa za kijilojia ambapo taarifa za madini ya kimkakati zikiwa kivutio kwake kutokana na nchi hiyo kupiga hatua kubwa kwenye masuala ya utengenezaji wa vifaa vya kiteknolojia vinavyotumia madini hayo.

Kwa mujibu wa taarifa za wizara na kampuni ya Lindi Jumbo inayotarajiwa kuzalisha madini ya kinywe wilayani Ruangwa, zinaonesha kuwa kuna kiwango cha tani zipatazo milioni 5.0 za mbale za madini hayo katika eneo hilo ambazo zinatarajiwa kuzalishwa kwa kipindi cha miaka 20 ya uhai wa mgodi.
Aidha, Tanzania imeonesha kuwa na hazina kubwa ya madini ya nikeli ambayo ni miongoni mwa madini ya kimkakati ambayo kiasi chake kinakadiriwa kufikia tani milioni 1.86 ikiwa ni nikeli ya daraja la kwanza yenye kiwango cha 3.44%. Madini hayo yanayotarajiwa kuchimbwa na kampuni ya Tembo Nickel wilayani Ngara mkoa wa Kagera na uhai wa mgodi unatarajia kuchukua takribani miaka 40.

Dhahabu ya Tanzania ilionekana kuwavuta wafanyabiashara na wawekezaji wengi katika maonesho hayo ambapo kampuni mbalimbali zilionesha nia ya wazi ya kuinunua na kuwekeza. Aidha mfumo wa masoko ya madini yaliyoanzishwa kote nchini ukionekana kuwa kichocheo kutokana na uhakika wa kufanya biashara pasipo kuwa na udanganyifu.

Kwa mujibu wa taarifa za wizara, Tanzania ni miongoni mwa nchi nne Barani Afrika zinazozalisha dhahabu kwa wingi, huku Mkoa wa Geita ukiongoza kwa uzalishaji, ambapo asilimia 40 ya dhahabu inayozalishwa nchini, inatoka Mkoani humo, ikifuatiwa na Wilaya ya Chunya. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa mikoa ya kanda ya Ziwa inaongoza kwa utajiri huo wa dhahabu.

Takwimu za Tume ya Madini zinazoonesha madini yaliyosafirishwa kwenda Dubai mara baada ya ushiriki wa Sekta ya Madini katika maonesho hayo katika kipindi cha mwezi Novemba 2021 hadi Aprili 2022, ni



pamoja na madini ya almasi yenye uzito wa karati 7,445.96 ya thamani ya shilingi 4,523,914,431.55; kilo 8,022.66 za dhahabu zenye thamani ya shilingi 968,589,888,771.73; tanzanite zenye uzito wa karati 1,058.33 zenye thamani ya shilingi 446,748,453.20, madini mengine ya vito yenye uzito wa karati 33.29 , vito vingine vyenye uzito wa gram 293.80 zenye thamani ya shilingi 8,233,787.47 na makinikia ya madini ya bati yenye uzito wa tani 76.04 ya thamani ya shilingi 5,255,209,376.53 yalisafirishwa kwenda Dubai.

Ukiachia mbali utajiri wa rasilimali madini zilizopo nchini, Madini ya Tanzania yana hadhi ya juu duniani kwa kuwa nchi ni ya amani, uchimbaji madini unazingatia misingi yote ya uchimbaji salama kwa kutochochea vita au migogoro, kuheshimu haki za binadamu, na kuepuka ajira za watoto.

Aidha, mazingira mazuri ya kiuwekezaji yaliyopo kwenye sekta ya madini, hali ya kisiasa, usalama na miundombinu inayoiunganisha Tanzania na nchi nyingine ni miongoni mwa masuala yanayoibeba Sekta ya Madini Tanzania kiuwekezaji na hivyo wawekezaji wengi kuwa na imani na kuvutiwa kuwekeza. Miongoni mwa miundombinu iliyopo na inayoendelea kujengwa nchini Tanzania ni ujenzi wa reli ya kisasa na bwawa la kuzalisha nishati ya umeme wa kiasi cha Megawati 2,115 kwa kutumia maji.



# USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA UCHUMI WA MADINI UNAVYOPEWA KIPAUMBELE SEKTA YA MADINI

**Na Tito Mselem**

Ushiriki wa Wananchi katika uchumi ni suala linalopewa kipaumbele katika Mataifa mengi Ulimwenguni, ili kuwezesha kupiga hatua za kimaendeleo hususan katika kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi unahusisha Jamii na Wananchi kiujumla hivyo, dhana ya local content ni muhimu sana.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan imeweka dhamira ya dhati kwa kuhakikisha uchumi wa Watanzania hususan katika miradi ya Sekta ya Madini inahusisha na kusimamiwa na Watanzania wenyewe kwa sababu ni nyenzo na chachu muhimu ambayo ina manufaa mapana kwa Serikali na jamii kwa ujumla.

Baada ya mabadiliko ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, suala la Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini limekuwa na umuhimu na la kuzingatia katika shughuli zote za mnyororo mzima wa thamani wa madini nchini, kwa lengo la kuweka usimamizi thabiti katika utekelezaji wa masuala yote ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini nchini.

Hivi karibuni, Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini iliandaa Jukwaa la Kwanza la Utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini lililofanyika jijini Mwanza kwa lengo la kuwaongezea uwezo watoa huduma wa Kitanzania ili waweze kuchukuwa fursa mbalimbali zilizopo katika Sekta ya Madini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini Adolf Ndunguru wakati anafunga jukwaa hilo anasema kuwa ni matarajio yake, jukwaa hilo linaweza kutoa ufumbuzi wa changamoto zote zilizopo kwenye Ushirikishwaji wa Watanzania kwa kiasi kikubwa na kuimarisha watoa huduma wa kitanzania, ili kuleta manufaa kwa watoa huduma wa Tanzania.

Ndunguru anasema Wizara ya Madini itaendelea na usimamizi thabiti kwa lengo la kuhakikisha kuwa, kipaumbele kinatolewa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na huduma zinazotolewa na Watanzania.

“Usimamizi huu wa utekelezaji wa Ushirikishwaji wa watanzania umepelekea kuibua na kuchochea kuongezeka kwa fursa mbalimbali katika nafasi za ajira na mafunzo, uhawilishwaji wa teknolijia, utafiti na maendeleo, matumizi ya huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinazotolewa na

Watanzania ambapo suala hili limepelekea Sekta ya Madini kuwa na mchango mkubwa nchini katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuwa fursa nyingi zinatolewa kwa watanzania na kuwapa nafasi ya kukuwa kiuchumi na kiteknolojia," anasema Ndunguru.

Aidha, matumizi ya huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinazotolewa na watanzania yamepelekea kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia malipo ya kodi na tozo mbalimbali katika utoaji wa huduma na bidhaa husika.

Inaelezwa kuwa, katika kipindi cha kuanzia Mwaka 2018 hadi 2021 Sekta ya Madini imeongeza kwa kiasi kikubwa kiwango cha Ushirikishwaji wa Watanzania katika maeneo mbalimbali kama vile ajira na mafunzo ambapo ajira kwa Watanzania katika migodi mikubwa na ya kati zimeongezeka kutokea 6,668 sawa na asilimia 95 kwa Mwaka 2018 hadi kufikia 14,308 sawa na asilimia 97 kwa Mwaka 2021 ya ajira zote. Ongezeko hili la ajira kwa Watanzania limechochewa na usimamizi imara wa Ushirikishwaji wa Watan-




Mwenyekiti wa Tume ya Madini Prof. Idris Kikula akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa Wizara ya Madini na Taasisi zake katika ufunguzi wa jukwaa la kwanza la Ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya Madini jijini Mwanza.



Baathi ya wafanyakazi wakiendelea na shughuli za uchenjuaji wa madini ya dhahabu katika kituo cha mfano cha Lwamgasa kilichopo Mkoani Geita.

zania ambapo Watanzania wanapewa kipaumbele.

Aidha, katika nafasi ambazo Watanzania hawajaweza kupata uzoefu kutokana na uwepo wa teknolojia mpya nchini, kumekuwa na utaratibu wa kuwa na mpango wa uhaulishaji wa teknolojia kwa Watanzania kwa nafasi zinazoshikiliwa na raia wa nchi nyingine.

Usimamizi huu umepelekea kuongezeka kwa idadi kubwa ya Watanzania wanaoshikilia nafasi za uongozi katika makampuni ya uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini. Aidha, Idadi kubwa ya Watanzania katika Sekta ya Madini wameweza kunufaika na mafunzo mbalimbali, mafunzo hayo yamepelekea kuwajengea uwezo wa utendaji kazi hususan zile ambazo zilikuwa hazifanywi na Watanzania kwa kiasi kikubwa.

Kufuatia matakwa ya Sheria ya Madini katika Ushirikishwaji wa Watanzania takwimu zinaonesha kuwa, manunuzi ya bidhaa na huduma, kwa kipindi cha kuanzia Mwaka 2018 hadi Mwaka 2021 kumekuwa na ongezeko la kiwango cha manunuzi ya bidhaa na huduma zilizotolewa na Watanzania na Kampuni za Kitanzania kwenye shughuli zinapo fanyika uchimbaji wa Madini. Katika Mwaka 2018 kilikuwa ni jumla ya Dola za Kimarekani milioni 238.71 sawa na asilimia 46 ya manunuzi yote, na Mwaka 2021 kufikia jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 2.104 sawa na asilimia 97 ya manunuzi yote. Aidha kumekuwa na ongezeko la idadi ya Watoa huduma Watanzania na Kampuni za Kitanzania ambapo kwa Mwaka 2021 jumla yake ilifikia 961 sawa na asilimia 61 ya watoa huduma wote katika kipindi hicho. Kupitia ongezeko hili ni wazi kuwa, usimamizi wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika fursa za kibiashara zilizopo katika Sekta ya Madini umenufaisha idadi kubwa ya Watanzania na kampuni za Kitanzania.

Naye, Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini Mhandisi Yahya Samamba anasema, uelewa wa masuala ya Ushirikishwaji wa Watanzania Katika kipindi cha kuanzia Mwaka 2018 hadi 2021 umeongezeka kwa kiasi kikubwa na kuchochea wadau wengi katika Sekta ya Madini kutimiza matakwa ya Kisheria. Uelewa umeongezeka miongoni mwa Watanzania kwa kuona fursa mbalimbali ambazo wanaweza kuzichukua na kuwanufaisha pia, uelewa wa kampuni za kigeni umeongezeka na baadhi ya kampuni hizo zimekwisha kukamilisha uwasilishaji wa mipango ya Ushirikishwaji wa Watanzania na uundaji wa Kampuni za ubia na Kampuni za Kitanzania.

Pamoja na mafaniko hayo, kumekuwepo na changamoto kadhaa kufuatia uwepo wa suala la Ushirikishwaji wa Watanzania ambazo ni pamoja na baadhi ya kampuni za kigeni kutokuwa tayari kufanya ubia na kampuni za kitanzania, upungufu wa viwanda vikubwa nchini kwa ajili ya uzalishaji wa vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji wa Madini, wamiliki wa leseni na watoa huduma kutotekeleza ipasavyo wajibu wao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, baadhi ya waajiriwa kushindwa kufanya kazi na kufikia ubora unaohitajika ili kurithi nafasi zinazoshikiliwa na wageni, Watanzania kuweka bei za bidhaa na huduma zilizopitiliza kwa kiasi kikubwa kuliko bei halisi ya soko.





# WACHIMBAJI WADOGO WALIVYOWEZESHWA KIELIMU, MITAJI, HUDUMA

**Na Steven Nyamiti**

Katika kuhakikisha wachimbaji wadogo wanakua, wanachimba kwa tija na kuchangia ipasavyo katika Pato la Taifa, Serikali kupitia Wizara ya Madini imeendelea kuzihamasisha taasisi za fedha na benki nchini kuwakopesha wachimbaji wadogo kwa wakubwa ili kuongeza tija katika shughuli zao.

Tayari benki kadhaa zikiwemo NMB, NBC, CRDB na KCB zimeanza kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo huku wizara ikiendelea kuzihamasisha taasisi hizo kuona uwezekano wa kuwakopesha vifaa.

Akiwasilisha bajeti yake Bungeni mwishoni mwa mwezi Aprili, 2022, Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko anasema hadi sasa taasisi hizo zimetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 36 kwa wachimbaji wadogo nchini.

Aidha, Dkt. Biteko anasema mbali ya mikopo, wizara kupitia taasisi zake za Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ziliwajengea uwezo kupitia mafunzo ambapo wachimbaji wadogo wapatao 1,144 walipata fursa ya kutembelea vituo vya mfano vya Katente na Lwamgasa vilivyopo mkoani Geita na Itumbi kilichopo wilayani Chunya. Vituo hivyo vinatoa mafunzo kuhusu uchimbaji bora, utafiti wa madini, biashara ya madini na uchenjuaji bora. ” Pia, wizara imetoa nakala zipatazo 1,000 za Mwongozo wa Wachimbaji wadogo, anasema Dkt. Biteko.

Mbali ya kutolewa mafunzo hayo, GST na STAMICO kushirikiana walitoa mafunzo ya vitendo kwa wachimbaji wadogo wapatao 945, wakiwemo wenye usikivu hafifu ili kuwawezesha kufanya uchimbaji wenye tija. Aidha, mada zilizotolewa

zililenga kuwafanya wachimbe kwa tija na msukumo ukiwekwa katika maeneo ya uchimbaji salama, biashara ya madini na namna bora ya uchukuaji sampuli. Mafunzo hayo yalitolewa katika maeneo ya Nh'oli (Dodoma), Mirerani, Chunya, Simiyu, Geita na Mwanza.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji mdogo zinaendelea kufanyika kwa ufanisi, Serikali imeendelea kuwarasimisha wachimbaji wadogo kuwawezesha kuchimba bila kubahatisha. Haya yanabainishwa pale GST ilipofanya utafiti maalum wa jiofizikia na jiokemia katika maeneo ya wachimbaji wadogo wilayani Biharamulo ambapo matokeo yalibaini uwepo wa madini ya kaolini na dhahabu.

Katika kuhakikisha wachimbaji wanachimba kitaalam na kwa tija ikiwemo kupata huduma mbalimbali kwa urahisi, GST ilifungua Ofisi yake mkoani Geita ili kusogeza huduma mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wadogo ikwemo za uchambuzi wa sampuli za maabara, utafiti, ushauri elekezi yote yakilenga kuwafanya wafanye shughuli zao kwa faida.

Aidha, katika kuhakikisha watanzania wengi wanashiriki katika shughuli za madini, wizara kupitia Tume hadi kufikia mwezi Machi 2022, ilitoa leseni 5,937 za uchimbaji mdogo wa madini, sawa na asilimia 72.65 ya leseni zote zilizotolewa ikilinganishwa na leseni 3,540 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2021.
kufuatia kurasimishwa na kutambuliwa kwa wachimbaji wadogo, mchango wao umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 4 kabla ya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 hadi asilimia 30 kwa sasa.

Akizungumzia mipango ya wizara katika kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo, kupitia hotuba yake bungeni, Dkt. Biteko anasema katika Mwaka wa Fedha 2022/23 wizara imepanga kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo na kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo yana taarifa za msingi za kijiolojia pamoja na kutoa huduma za utafiti kwa gharama nafuu.

“Wizara imekusudia kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwafanya waweze kukua kutoka uchimbaji mdogo na kuwa wachimbaji wa kati na baadaye kuwa wachimbaji wakubwa kwa kuwapatia mafunzo yanayohitajika kuhusu uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini,” anasisitiza Dkt. Biteko.

Ama kwa hakika juhudi za kuendelea kuwaendeleza wachimbaji wadogo zimefanyika hivyo, wachimbaji hawana budi kuzingatia Sheria na taratibu zinazowaongoza kufanya kazi kwa maendeleo ya sekta ya Madini.



Wachimbaji wadogo wenye usikivu hafifu kutoka Geita wakifurahia vifaa vya uchimbaji kutoka STAMICO.




# MAKAA YA MAWE YA KUPIKIA MWAROBAINI ATHARI ZA MAZINGIRA

Na Tito Mselem

Pamoja na Serikali kuendeleza juhudi za kupambana na matumizi ya mkaa utokanao na misitu na badala yake kutumia nishati mbadala kama makaa ya mawe kwa ajili ya kupikia, bado kuna jamii kubwa ambayo inauelewa mdogo kuhusu nishati hiyo.

Katika kukabiliana na tatizo la ukataji miti na kulinda mazingira, Serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), imejenga na kusimika miundombinu na mitambo ya kuzalisha makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya nyumbani unaojulikana kama Rafiki coal briquetters ambao ni mwarobaini wa kupambana na janga hilo.

Aidha, katika kuhakikisha kunakuwa na uzalishaji wa kutosha kukidhi mahitaji, STAMICO imeagiza mitambo miwili yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 za makaa hayo kwa saa. Kiwanda cha kuzalisha mkaa huo kimejengwa eneo la TIRDO jijini Dar es Salaam na kuna mpango wa kujenga mtambo kama huo Mkoani Songwe.

Kwa mujibu wataarifa ya STAMICO, mradi huo unatarajia kuwanufaisha watanzania kwa kutoa ajira zaidi ya 200 na kupunguza ukataji miti kwa ajili ya mkaa hivyo kuchangia kutunza mazingira.

Wakichangia kuhusu ubora wa makaa hayo wajumbe wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini baada ya Kaimu Mkurugenzi Mtendajiwa STAMICO Dkt. Venance Mwasse kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya mradi huo, wajumbe hao wanakiri kuhusu ubora wa makaa hayo baada ya kuyajaribu na wanaitaka wizara kuharakisha mchakato wake.

Tayari STAMICO imeanza kusambaza nishati hiyo ambayo inatajwa kuwa nafuu zaidi na rafiki kwa mazingira baada ya kuidhinishwa na Shirika la Viwango la Taifa (TBS) tayari kwa matumizi baada ya uzalishaji wa majaribio kufanyika kwa ufanisi.

Aidha, Mkaa huo unaelezwa kuwa na faida lukuki na baadhi zinatajwa kuwa ni pamoja na rafiki wa mazingira, kuokoa pesa nyingi zinazotumika kwenye nishati nyingine, mkaa wa mawe wakupikia unadumu jikoni kwa muda mrefu kuliko mkaa wa miti hivyo kuzidi kupunguza gharama za matumizi ya nishati hiyo, huboresha usafi wa jikoni na maeneo ya nyumbani yanayochafuliwa na mkaa wa miti.

Pia, inaelezwa kuwa, vyombo vya kupikia vinavyochafuliwa na mkaa wa msituni havichafuki kutokana na matumizi ya mkaa wa mawe, ambapo pia majivu ya mkaa huo hutumika kwa kurutubisha ardhi shambani, wanasayansi wamebainisha kuwa majivu ya mkaa wa mawe yanaviinilishe vya mimea, yakiwamo mazao mbalimbali yanayostaw-

ishwa na wakulima.

Baadhi ya watumiaji katika jiji la Dodoma ambao wametumia mkaa huo wanakiri kuwa kilo moja ya briketi inatoa nishati jikoni si chini ya saa sita na kuendesha mapishi mbalimbali mfululilzo.

Mmoja wa watumiaji wa briketi ambaye ni mkazi wa Kisasa jijini Dodoma Josephine Tenga, anasema amevutiwa na matumizi ya briketi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwake sababu yamempunguzia gharama kubwa alizokuwa anagharamika kununua mkaa unaotokana na miti hapo awali.

"Pale nyumbani tunatumia mkaa wa mawe kwa kupikia mapishi mbalimbali, nimefurahishwa sana jinsi mkaa huu unavyo hifadhi moto mkali kwa muda mrefu wa takribani saa sita tunapikia maharage au kande na vyakula vingine lakini moto unabaki," anasema Tenga.
Tenga anasema familia yake imegundua kuwa, matumizi ya gesi na mkaa wa miti unagharimu sana kuliko matumizi ya mkaa wa mawe. Anasema mkaa wa mawe pia hudhibiti uchafu wa jikoni na ni rahisi kusafisha jiko.

Akielezea faida za mkaa huo, Tenga anasema "Miongoni mwa faida za makaa haya ya mawe ni pamoja na unafuu wa bei katika manunuzi, kwa mfano tani moja ya mkaa wa miti ni shilingi 2,225,000 lakini mkaa huu unaotokana na makaa ya mawe tani moja ni shilingi 1,500,000 ukiagiza kutoka kiwandani," anasema.

Anafafanua kuwa, makaa ya mawe kwa bei ya rejareja huuzwa shilingi 2000 kwa kilo ambapo kwa kilo moja ya mkaa huo unaweza ukapikia vitu vingi kwa kuwa toka kuwaka kwake mpaka kuwa jivu huchukua zaidi ya masaa sita mpaka manane.

Kwa upande wake, Frank Shija mkazi wa Meliwa jijini Dodoma, mawe kupikia wamegundua faida nyingi za kiuchumi kwa kuwa hutumia kiasi kidogo cha fedha katika nishati hiyo kuliko walivyokuwa wakitumia nishati ya mkaa utokanao na misitu hapo awali.

"Nilikuwa natumia karibu 4,000 kila siku kununua mkaa wa miti wa rejareja, kwa wiki mbili ilinigharimu shilingi 56,000. Kwa sasa natumia nishati ya makaa ya mawe kupikia ambapo kwa wiki mbili natumia kilo 14 ambazo zinanigharimu kiasi cha shilingi 28,000 tu," anasema Shija.

Mbali na manufaa hayo ya mkaa wa mawe, wanamazingira wameshabainisha kutoweka kwa misitu katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara kutokana na matumizi ya miti kwa ajili ya nishati na shughuli nyingine za kiuchumi, pia wanasema matumizi ya makaa ya mawe kwa nishati ya kupikia yataokoa misitu mingi.

Misitu inatajwa kuwa muhimu kwa maisha ya binadamu na viumbe hai kwa kua huifadhi vyanzo vya maji, kuboresha hali ya hewa, kuzuia mmomonyoko wa ardhi, mbao, madawa, malisho ya mifugo, kuboresha shughuli za kilimo na kuboresha
mandhari ya nchi yetu mijini na vijijini, hivyo matumizi ya mkaa wa miti kwa kuwa hayana faida kiuchumi na athari zake kimazingira ni kubwa ukilinganisha na makaa ya mawe ambayo matumizi yake ni rahisi na hupika kwa haraka zaidi na yana faida nyingi kuliko matumizi ya mkaa wa miti ambapo matumizi ya nishati mbadala yanatajwa kama moja ya suluhisho la tatizohilo.

Kutokana na manufaa ya mkaa huo, tayari STAMICO inaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa jamii kubwa inanufaika na inatumia mkaa huo ambao ni wazi utasaidia kufanikisha kampeni ya utunzaji wa misitu.



Baadhi ya Makaa ya Mawe yakiwa yamekusanywa pamoja yaliyochimbwa na kampuni ya TANCAOL mkoani Ruvuma.

# WIZARA ILIVYOSHIRIKI MAADHIMISHO YA MEI MOSI












# WIZARA ILIVYOSHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI










# USHIRIKI WA WIZARA MICHEZONI















www.madini.go.tz